OFISI YA RAIS

# UTUMISHI

NA UTAWALA BORA



## MATUKIO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA - 2024

1

# WAZIRI SIMBACHAWENE ATOA RAI KWA WANANCHI KUTUMIA MIFUMO YA TEHAMA YA SERIKALI




*— na Veronika na Lusungu Helela*
*Dodoma*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene ametoa rai kwa wananchi kuwa wafuatilliaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika simu zao za kiganjani ili kujipatia huduma nyingi za kijamii zitolewazo na Serikali

Ametoa kauli hiyo leo Jumatano Julai 19, 2024 wakati akifungua Maadhimisho na Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyoanza Juni 16 katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.

Mhe. Simbachawene amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza matumizi ya TEHAMA katika kuwawezesha wananchi kupata huduma zitolewazo na Serikali kwa haraka, uwazi na bila kuwa na urasimu

Kufuatia hatua hiyo amesisitiza wananchi kutumia simu zao ili kupata huduma hizo badala ya kujikita kuangalia pekee michezo ya kubashiri na tamthilia kupitia simu zao za kiganjani

Amesema lengo la kuhakikisha huduma za serikali zinapatikana kupitia simu za kiganjani ni kuona wananchi wanapata huduma bora zenye gharama nafuu na kwa haraka katika mikoa na wilaya zote tofauti ilivyokuwa miaka ya nyuma.




Wakati huo huo, Mhe.Simbachawene amewataka Watumishi wa Umma kutumia mifumo ya TEHAMA iliyobuniwa na Serikali ili kurahisisha utoaji huduma na kuondoa malalamiko kwa wananchi wanaowahudumia

Katika hatua nyingine Mhe. Simbachawene amewataka watumishi ambao hawajajisajili na kujaza mipango kazi katika Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) wawe wamekamilisha kabla ya wiki ijayo ili kila mmoja awe ameingia kwenye mfumo huo.

“Kabla sijahitimisha hotuba yangu nitoe maelekezo yafuatayo, Watendaji wote wahakikishe watumishi ambao bado hawajajisajili kwenye Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) wawe wamefanya kazi hii ili mpaka wiki ijayo jambo hili liwe limeshakwisha kabisa na kila mmoja awe ameingia kwenye mfumo.” Amesema Mhe. Simbachawene.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kitaifa yanaratibiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo kwa mwaka huu, Wizara na Taasisi mbalimbali za serikali zinatoa huduma za papo kwa hapo ikiwemo hati za viwanja, vitambulisho vya uraia na huduma nyinginezo katika Viwanja vya Chinangali Park.

*PICHA: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kuhusu Mifumo ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Sera za Tehama na Viwango, Bw. Ibrahim Toure wakati alipotembelea banda la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene akifurahia jambo na Naibu Waziri wa Ofisi yake Mhe. Ridhiwani Kikwete (kushoto) na Mkurugenzi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Bw. Firimin Msiangi wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma*



*Sehemu ya Wananchi na Watumishi wa Umma, wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo kitaifa yamefanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene akipata maelezo kutoka kwa Mtumishi wa Wizara ya Nishati wakati alipotembelea banda la Wizara hiyo kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*

# 2 WAZIRI MKUU MHE. KASSIM MAJALIWA ATAKA MPANGO MKAKATI WA MATUMIZI WA MIFUMO YA KIDIGITALI KATIKA UTUMISHI WA UMMA



*— na Veronika na Lusungu Helela*
*Dodoma*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amezitaka Taasisi za Umma kuweka mipango madhubuti ya kutumia mifumo ya kidijitali ambayo italeta mageuzi ya kiutendaji na kuifanya Tanzania kuendana na mapinduzi ya nne ya viwanda yanayotumia TEHAMA.

Ametoa kauli hiyo leo hivi karibuni jijni Dodoma katika viwanja vya Chinangali Park wakati akimwakilisha Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyosanifiwa na kujengwa na Ofisi ya Rais-UTUMISHI.

Amezitaka Taasisi hizo kufuatilia na kuhimiza matumizi ya mifumo hiyo kwa Watumishi wanaowaongoza.

Amesema uzinduzi wa mifumo hiyo ya kidijitali ni utelelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambapo Serikali itaweza kuwahudumia wananchi kwa uwazi na kwa haraka zaidi.

Ameitaja mifumo iliyozinduliwa kuwa ni HR Assesment, PEPMIS na PIPMIS, e-Watumishi (HCMIS) pamoja na e-Mrejesho.

Amesema mifumo hiyo ikitumika ipasavyo itasaidia kuwabaini Watumishi mahiri na watumishi wazembe pamoja na kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utumishi wa umma.

"Mifumo hii ikitumiwa kama ilivyokusudiwa itasaidia kuwabana Watumishi wazembe na hivyo kuongeza uwazi uwajibikaji na ufanisi katika kuwahudumia wananchi " amesisitiza Mhe.Majaliwa

Katika hatua nyingine Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amewapongeza vijana wazawa kwa ubunifu wa kusanifu mifumo hiyo huku akiutaja mfumo wa e-Mrejesho uliotambulika kimataifa kutokana na ubora wake.

Akizungumzia Wiki ya Utumishi wa Umma amesema moja ya lengo lake ni kuhimiza uwajibikaji, uwazi, uadilifu pamoja na utoaji huduma bora kwa wananchi

"Hongereni sana Taasisi za Umma kwa utayari wenu wa kutoa huduma kwa wananchi kuanzia Juni 16 hadi leo hii siku ya Kilele" amesisiiza Waziri Mkuu.

Amesema kitendo cha kufanyika kwa maonesho hayo ni dalili tosha kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imejizatiti kutoa huduma bora za papo kwa hapo kwa wananchi pasipo wananchi kulazimika kuzifuata huduma hizo maofisini.

Kwa upade wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ys Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amesema matumizi ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma yameondoa usumbufu, rushwa pamoja na kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Amesema mifumo hiyo imesanifiwa na kujengwa na wazawa ukiwemo mfumo wa e-Watumishi (HCMIS) ambao una uwezo wa kuhifadhi taarifa za watumishi wa umma kuanzia siku aliyoajiriwa hadi siku ya kustaafu.

Amesema mfumo wa upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi na taasisi PEPMIS na PIPMS umesaidia kuondoa upendeleo na uonevu na unahamasisha utendaji kazi miongoni mwa watumishi.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, UTUMISHI, Bw.J uma Mkomi amesema matumizi wa Mifumo ya Utendaji Kazi ikiwemo PEPMIS na PIPMIS imeonekana kuwa ni kikwazo kwa baadhi ya Watumishi kwa sababu Watumishi wengi hawapendi kubanwa.

Bw. Mkomi amesema mtumishi yeyote ambaye hatojaza majukumu yake kwenye mfumo huo hatopata ruhusa ya kuhama wala kwenda masomoni pamoja na kutopanda cheo.

Katika hatua nyingine Bw. Mkomi amesema Mfumo wa e-mkopo umewarahisishia Watumishi wa Umma kupata mkopo kwa haraka na pia mfumo huo hautoi fursa kwa Watumishi kukopa benki nyingine endapo Mtumishi atakuwa na mkopo katika benki nyingine.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala Bora, Mhe. Frolent Kyombo ameipongeza Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa usanifu na kujenga mifumo hiyo ya Kidijitali kwani imesaidia kupunguza usumbufu na gharama kwa watumishi wa Umma wa kufuatilia huduma Dodoma.




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kuhusu Mifumo ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Sera za Tehama na Viwango, Bw. Ibrahim Toure wakati alipotembelea banda la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akipiga makofi mara baada ya kuzindua Mifumo ya Utendaji Kazi Serikalini wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma. Wengine ni Viongozi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Watendaji wengine wa Serikali.*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akipiga makofi mara baada ya kuzindua Mifumo ya Utendaji Kazi Serikalini wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma. Wengine ni Viongozi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Watendaji wengine wa Serikali.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Afisa Mhifadhi Mkuu wa Malikale Bw. William Mwita wakati alipotembelea banda la Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Uzinduzi wa mifumo ya kidijitali iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*




# 3 IFAHAMU HISTORIA YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni siku maalum ya Watumishi wa Umma ambayo husherehekewa tarehe 23 Juni kila mwaka na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) kwa lengo la kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika maendeleo ya Nchi zao na Bara la Afrika kwa ujumla. Chimbuko la Sherehe hizi ni uamuzi wa Mkutano wa Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma uliofanyika Tangier Nchini Morocco mwaka 1994.

Aidha, Mkutano wa nne wa Mawaziri wenye dhamana na Utumishi wa Umma Barani Afrika uliofanyika Mwezi Mei 2003 uliamua kuwa Siku ya Utumishi wa Umma iwe ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma chini ya Umoja wa Afrika (AU).

katika kufikia Siku ya Utumishi wa Umma, shughuli mbalimbali hufanyika ikiwemo Watumishi wa Umma kufanya maonesho kwa malengo yafuatayo;

i. Kutambua mchango na umuhimu wa Watumishi wa Umma katika kuleta maendeleo kwenye Nyanja mbalimbali za maendeleo katika Mataifa yao;

ii. Kuwezesha Watumishi wa Umma kutambua Dira, Dhima, na Malengo; Programu na Mikakati; na Mafanikio na Changamoto zinazokabili Utumishi wa Umma;

iii. Kuhamasisha na kuwapa motisha Watumishi wa Umma waendelee na kazi yao nzuri ya ujenzi wa Taifa na kuendelea kuwa wabunifu ili kutatua changamoto mbalimbali katika jamii;

**iv.** Kupata mrejesho kutoka kwa wateja/wananchi na wadau wanaowahudumia; na

**v.** Kuandaa Utumishi wa Umma ili uweze kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo siku za



*PICHA: Wakuu wa Taasisi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Viongozi wa dini wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma uliofanyika Jijini Dodoma.*

Ndugu Viongozi na watumishi wa umma, zipo faida nyingi zinazotokana na Siku ya Utumishi wa Umma, miongoni mwa faida hizo ni zifuatazo;

**i.** Wananchi kupata fursa ya kufahamu wajibu wao na haki ili pindi wanapokosa haki zao waweze kujua namna ya kuzipata.

**ii.** Taasisi za Umma kupata fursa ya kubadilishana uzoefu juu ya mbinu na mikakati mipya ya namna ya kutoa huduma bora kwa Umma;

**iii.** Taasisi za Umma kupata fursa ya kuonesha ubunifu waliofanya katika maeneo mbalimbali ya utoaji huduma na kuondoa urasimu usiokuwa wa lazima katika michakato mbalimbali ya utoaji huduma;

**iv.** Taasisi za Umma kupata fursa ya kupokea ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wananchi, AZAKI, na Sekta Binafsi juu ya namna bora ya kuboresha utoaji huduma na;

**v.** Taasisi za Umma kupata mrejesho na kuutumia mrejesho huo kurekebisha kasoro za kiutendaji zinazosababisha malalamiko ya Wananchi (wateja) ili huduma za Serikali ziboreshwe na kukidhi matarajio ya Wananchi ambao ni walipa kodi wetu.

# 4 TANZANIA YANG'ARA TUZO ZA KIMATAIFA ZA UBUNIFU WA MFUMO WA KIDIJITALI WA E-MREJESHO

*— na Mwandishi Wetu, Korea*

Tanzania imeng'ara katika tuzo za Kimataifa za ubunifu wa mfumo ya kidijitali wa Mrejesho (e-Mrejesho) uliosaidia kuleta mageuzi makubwa katika uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Tuzo hizo zimetolewa jana nchini Korea na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) wakati wa Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma ( 2024 UN Public Service Awards (UNPSF) ikiwa ni muendelezo wa Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofikia kilele chake Juni 23 Mwaka huu.

Tuzo hiyo iliyopokelewa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi ambapo nchi 15 kati ya 72 zimetunukiwa tuzo hizo huku kwa upande wa Afrika, Tanzania na Afrika ya Kusini ndizo zilizotambuliwa katika tuzo hizo.

Akizungumza mara baada ya kupokea tuzo hiyo, Naibu Katibu Mkuu, Bw. Daudi amesema Tanzania imepokea tuzo kwenye kipengele cha ubunifu kwenye Taasisi za Umma (Honorable Mention Innovation in Public Institution).

"Tuzo tuliyoipokea ni heshima kubwa na pia ni fahari kwa vijana wetu wazawa waliobuni mfumo huo ambao wananchi wana uwezo wa kuiambia Serikali yao kwamba utumishi wa umma una uimara na ulegevu katika utoaji huduma'', amesema.



*PICHA: Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi (wa tatu kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Wakurugenzi alioongozana nao nchini Korea Kusini wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kupokea tuzo za Kimataifa za ubunifu wa mfumo ya kidijitali wa Mrejesho (e-Mrejesho) ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Maadili, Bi. Leila Mavika (wa tatu kushoto) akiwa ameshika tuzo hiyo ambayo Tanzania imekabidhiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) wakati wa Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma ( 2024 UN Public Service Awards (UNPSF) Wa nne kulia ni Balozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini, Mhe. Balozi Togolani Mavura.*




*PICHA: Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi (wa tatu kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Wakurugenzi alioongozana nao nchini Korea Kusini wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kupokea tuzo za Kimataifa za ubunifu wa mfumo ya kidijitali wa Mrejesho (e-Mrejesho) ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Maadili, Bi. Leila Mavika (katikati) akiwa ameshika tuzo hiyo ambayo Tanzania imekabidhiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) wakati wa Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma (2024 UN Public Service Awards (UNPSF) Wa tatu kulia ni Balozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini, Mhe. Balozi Togolani Mavura.*

Katika mkutano huo ujumbe wa Tanzania umeongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi pamoja na Wakurugenzi kutoka Ofisi hiyo akiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Maadili Bi. Leila Mavika, Mkurugenzi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Serikalini, Bw. Priscus Kiwango pamoja na Mkurugenzi, Mhandisi Rico Bomani na Meneja wa Mafunzo na Ubunifu, Mhandisi Jaha Mvula kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi akitoa utambulisho wa Viongozi waliohudhuria kwenye Ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*



*Afisa Utumishi Mwandamizi Ofisi ya Rais-UTUMISHI Bi. Annajackline Muhuga akimhudumia mwananchi aliyefika kwenye banda la ofisi hiyo kwa lengo la kupata huduma ya kiutumishi wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano, Ofisi ya Rais-UTUMISHI Bi. Mary Mwakapenda akifafanua jambo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene pamoja na Viongozi wa ofisi hiyo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo kitaifa yamefanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma. Wapili kutoka kulia ni Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri.*




*Watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiwa katika picha mara baada ya kuwahudumia wananchi waliofika katika banda la ofisi hiyo wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa ameshika  zawadi ya asali aliyopewa mara baada ya kutembelea la Wizara ya Maliasili na Utalii  kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo kitaifa yamefanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa kwenye picha ya pamoja   Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe Mhe. Daniel Sillo wakati alipotembelea banda la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora  hiyo kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma. Kulia ni Katibu Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akiwa pamoja na baadhi Wakurugenzi ofisi hiyo na Wizara ya Mambo ya Ndani.*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akisaini kitabu wakati alipotembelea banda la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma. Kulia ni Katibu Ofisi ya Rais-UTUMISHI.*

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

# ASANTENI



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, **Bw. Juma Mkomi** anapenda kuzishukuru Wizara, Taasisi za Umma, Mabenki, Watumishi pamoja na jamii kwa ujumla, kwa kushiriki katika Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofanyika kuanzia Juni 16 hadi 23, 2024 katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma

Aidha, Bw. Mkomi anawashuruku Watumishi na Wananchi wote walioshiriki kwenye Uzinduzi wa Mifumo ya Kidijitali

**TUKUTANE 16-23 Juni, 2025**

ofisi_ya_rais_utumishi